# ziara ya mafunzo kwa wakulima

## kati ya kanda ya mashariki na ya nyanda za juu kusini



TARP II – SUA Project

**Waandishi**

Dk. J. G. Lyimo-Macha
Prof. E. K. Batamuzi
Prof. A. J. P. Tarimo

**Wahariri**

Kamati ya Mradi:

Prof. L. D. B. Kinabo
Prof. R. E. Malimbwi
Dk. P. J. Makungu

**ISBN9987 605 49 4**

**Kimechapishwa na:**

Mradi wa Uhakika wa Chakula na Pato la Kaya kwa
Wakulima Wadogowadogo, Tanzania (TARP II – SUA Project)
Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo
SLP 3151
Chuo Kikuu, Morogoro
Simu: +255 23 2600970 au +255 23 2603511 ext. 4251

Toleo Namba: TS 2-30

**© 2001 TARP II – SUA Project**

Mbunifu wa Jalada - L.D.B. Kinabo: Picha inawaonyesha akina mama wa Mbarali wakilima kwa maksai kama njia mojawapo ya kurahisisha kazi na kuongeza uzalishaji katika kilimo.



# Yaliyomo

*Dibaji* v

*Vifupisho* vii

**1.0 Utangulizi 1**

**2.0 Mifano Hai 2**

**2.1. Kanda ya Mashariki: Uzoefu Kutoka Wilaya ya Lushoto** 2

2.1.1. Vigezo vya kuchagua maeneo na wakulima 2

2.1.2. Matokeo 3

2.1.3. Mafunzo 4

2.1.4. Mipango ya utekelezaji ya wakulima 5

2.1.5. Hoja zilizojitokeza 6

2.1.6. Mapendekezo ya wawezeshaji 7

**2.2. Nyanda za Juu Kusini: Uzoefu kutoka wilaya za Njombe na Mbarali** 9

2.2.1. Vigezo vya kuchagua maeneo na wakulima 9

2.2.2. Matokeo 10

2.2.3. Mafunzo 11

2.2.4. Mipango ya utekelezaji ya wakulima 12

2.2.5. Hoja zilizojitokeza 13

2.2.6. Mapendekezo ya wawezeshaji 14

**3.0 Hitimisho 15**

# Dibaji

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo na Uhakika wa Chakula, pamoja na Chuo Kikuu cha Kilimo cha Norway (NLH), kinatekeleza Mradi wa Uhakika wa Chakula na Pato la Kaya kwa Wakulima Wadogo wadogo Tanzania.

Lengo mojawapo katika mradi huu ni kuimarisha uhusiano kati ya Wakulima, Watafiti na Washauri wa Ugani. Ili kufikia lengo hili, mradi umepanga utaratibu wa kuwawezesha wakulima kutembeleana ndani ya kanda zao na kati ya kanda na kanda.

Makala hii inawasilisha ripoti ya ziara mbili (kanda moja kwenda kanda nyingine) zilizofanyika mwezi Agosti na Septemba 2001. Ziara ya kwanza ya kimafunzo ya wakulima iliwashirikisha wakulima na washauri wa ugani kutoka wilaya za Mbinga, Njombe, Makete na Mbeya (Kanda ya nyanda za juu kusini) hawa waliwatembelea wakulima wenzao wa wilaya ya Lushoto. Ziara ya pili iliwajumuisha wakulima na washauri wa ugani kutoka wilaya za Bagamoyo, Morogoro Vijijini na Kilosa (Kanda ya Mashariki) ambao waliwatembelea wakulima wa wilaya za Njombe na Mbarali. Taarifa hii pia inapatikana katika lugha ya Kiingereza.

*Profesa L. D. B. Kinabo*
*Mratibu wa Mradi, TARP II-SUA*
*Oktoba 2001*

# Vifupisho

| | |
|---|---|
| ADT | Teknolojia zitokanazo na Wanyama Kazi |
| ARI | Taasisi ya Utafiti wa Kilimo |
| EZ | Kanda ya Mashariki |
| FYM | Samadi |
| HPI | Mradi wa Kimataifa wa Mitamba |
| IAT | Kamati ya Kutathmini Matokeo |
| M&E | Ufuatiliaji na Tathmini |
| MAFS | Wizara ya Kilimo na Uhakika wa Chakula |
| NLH | Chuo Kikuu cha Kilimo cha Norway |
| SACCOS | Vyama vya Kuweka na Kukopa |
| SECAP | Mradi wa Uzuiaji wa Mmomonyoko wa Udongo na Kilimo Mseto |
| SHZ | Kanda ya Nyanda za Juu Kusini |
| SUA | Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo |
| TARP II | Mradi wa Taifa wa Utafiti wa Kilimo Awamu ya Pili |

# 1.0. UTANGULIZI

Ili kukuza na kuendeleza mahusiano kati ya wakulima, watafiti na washauri wa wakulima, njia mbalimbali mbalimbali hutumika. Mojawapo ni ziara za mafunzo ambazo wakulima wanapata nafasi ya kutembeleana ndani ya kanda na kati ya kanda na kanda. Wakulima wakiandamana na washauri wao pamoja na watafiti kutoka kanda ya Nyanda za Juu Kusini waliwezeshwa kuwatembelea wenzao wa kanda ya Mashariki kuanzia tarehe 29 Agosti hadi 2 Septemba 2001. Vivyo hivyo wakulima na washauri wa kanda ya Mashariki waliwatembelea wenzao wa kanda ya Nyanda za Juu Kusini kuanzia tarehe 10 Septemba hadi 12 Septemba 2001.

Katika kanda ya Mashariki, wakulima, washauri wa ugani na watafiti toka maeneo yenye miinuko ya Nyanda za Juu Kusini waliwatembelea wenzao wa milima ya Usambara ili kubadilishana uzoefu katika hifadhi ya ardhi katika sehemu husika. Na huko Nyanda za Juu Kusini walipokea ugeni toka wilaya za Morogoro Vijijini, Bagamoyo na Kilosa ukiwajumuisha wakulima, washauri wa ugani pamoja na watafiti kwa madhumuni ya kubadilishana uzoefu katika utunzaji na utumiaji wa samadi, ufugaji bora na matumizi ya maksai kwa shughuli mbalimbali za kilimo.

## 2.0. MIFANO HAI

### 2.1. Kanda ya Mashariki: Uzoefu kutoka wilaya ya Lushoto

Wakulima pamoja na washauri wao toka wilaya za Mbinga, Mbeya, Njombe na Makete katika kanda ya Nyanda za Juu Kusini waliwatembelea wakulima walio katika mradi wa Uzuiaji Mmomonyoko wa Udongo na Kilimo Mseto (SECAP) katika vijiji mbali mbali vya wilaya ya Lushoto. Ziara hiyo ilifanyika kuanzia tarehe 29 Agosti hadi 2 Septemba 2001.

#### 2.1.1 Vigezo vya kuchagua maeneo na washiriki

*Uchaguzi wa eneo*:

Uchaguzi wa eneo la kutembelewa ulizingatia mada iliyotokana na matatizo makuu katika kilimo yaliyoanishwa wakati wa warsha ya kwanza ya wakulima Nyanda za Juu Kusini iliyofanyika huko Nazareth, Njombe mwishoni mwa mwaka 2000. Mada husika ilikuwa matatizo ya mmomonyoko na kupungua kwa rutuba ya udongo katika sehemu za miinuko. Lengo lilikuwa kutembelea maeneo ambapo teknolojia za kuhifadhi udongo zimepelekwa, kupokelewa na kutekelezwa kwa vitendo na wakulima katika eneo husika.



*Uchaguzi wa wakulima*:

Wakulima 12 walichaguliwa kwa kutumia vigezo vifuatavyo:
ubunifu; uhusiano na vikundi au vyama vya wakulima, uwezo wa kushirikiana na wenzake na jinsia. Kundi hili pia limekuwa na washauri wa ugani wawili, watafiti watatu kutoka Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) na mmoja kutoka Taasisi ya Utafiti Uyole (ARI).

#### 2.1.2 Matokeo ya Msingi

Wageni walitembelea sehemu mbali mbali za wilaya ya Lushoto na kushuhudia mbinu mbalimbali za hifadhi ya ardhi na mazingira. Kati ya walioyaona, wageni waliguswa na yafuatayo:

- Hifadhi ya ardhi:
  - Utengenezaji wa matuta ngazi na makinga maji.
  - Kilimo mseto.
- Kulisha/kufugia ng'ombe bandani kama mbinu ya kuhifadhi ardhi.
- Kulima mboga mboga katika mabonde wakati wa kiangazi.
- Kutengeneza na kutumia majiko yanayotumia nishati kidogo mfano jiko la *upesi*
- Umwagiliaji kwa kutumia mifereji ya asili
- Mgawanyo wa kazi zinazohusu uhifadhi ardhi, kilimo na masoko kati ya wanaume na wanawake
- Ujenzi wa nyumba bora

### 2.1.3 Mafunzo

Ziara hii ilikuwa ya mafanikio kwa wageni na wenyeji sawia. Wageni walijifunza mbinu bora za kuhifadhi ardhi na malisho kwa mifugo wakati wa kiangazi. Wenyeji walijifunza kuhusu ufugaji bora, utunzaji na matumizi bora ya samadi shambani.
Ili kujua kwa hakika wageni wamejifunza nini katika ziara, wakulima walitakiwa kueleza waliyojifunza wakati wa ziara. Kila mshiriki alitakiwa kuandika mambo matatu aliyojifunza.
Ifuatayo ni orodha ya yale waliyojifunza:

- Njia rahisi ya kutengeneza matuta ngazi na makinga maji kwa njia ya fanya juu.
- Kuunda na kuendeleza vyama / vikundi vya wakulima.
- Umuhimu wa kufugia ng'ombe bandani.
- Kilimo cha umwagiliaji kwa kutumia mifereji ya asili wakati wa kiangazi
- Umuhimu wa kutumia mabonde kwa kilimo cha mboga mboga wakati wa kiangazi.
- Matumizi ya dawa za asili zitokanazo na mimea kwa ajili ya kudhibiti wadudu na magonjwa ya mifugo na mazao.
- Kuunda na kuendeleza vyama vya kuweka na kukopa.



500316 48072



*Picha hii inamwonyesha mkulima wa Lushoto akitoa maelezo kwa wageni wake kutoka nyanda za Juu Kusini kuhusu ufugaji bora, utunzaji na matumizi bora ya samadi shambani*

### 2.1.4 Mipango ya utekelezaji ya wakulima

Ziara kama hizi zina umuhimu mkubwa kwa wakulima wadogo wadogo kwani huchangia katika kukuza ufahamu wa mbinu mbalimbali za kumkwamua mkulima kutokana na matatizo ya pato duni na uhaba wa chakula.

Ili kuweza kupima mafanikio ya ziara hii, kila mshiriki aliombwa kuandika mambo matatu ya kutekeleza arudipo nyumbani.
Yafuatayo ni yale yaliyoahidiwa kutekelezwa:

- Kutengeneza matuta ya ngazi
- Kufugia bandani.
- Kuanzisha kilimo cha mboga mboga katika mabonde kwa ajili ya chakula na kuongeza kipato.
- Kupanda miti kwa ajili ya kuhifadhi ardhi
- Kutengeneza na kutumia jiko la upesi
- Kulima kilimo cha kiangazi kinachotegemea umwagiliaji
- Kuhifadhi misitu ya asili
- Kuunda na kutumia miti asili na vichaka au nyasi kwa ajili ya dawa za mifugo na mimea.

### 2.1.5 Hoja zilizojitokeza

Kutokana na waliyoyaona, wakulima walitoa hoja kwa ajili ya kuboresha ziara kama hizi ili kuongeza mafanikio. Wakulima walidokeza kuwa kulikuwa na mambo muhimu yaliyosahaulika katika ratiba iliyotolewa kuongoza ziara. Kwa mfano, ufugaji wa samaki na nyuki. Wakulima walitoa hoja zifuatazo:

- Hawakupendezwa na jinsi wenyeji walivyokuwa:
    - Wanatunza ng'ombe wao, hasa katika ujenzi wa mabanda na malisho.
    - Wanatunza samadi
- Wakulima wawezeshwe katika;
    - Kutekeleza kilimo mseto
    - Kuunda na kutumia majiko aina ya *upesi*
    - Kuunda vikundi vya wakulima vya kuweka na kukopa.
    - Ziandaliwe ziara nyingi zaidi
    - Viandaliwe vipeperushi kuhusu yale walioyaona / kujifunza wakati wa ziara.
    - Wakulima watembelewe ili kuangalia na kuthibitisha yale waliyojifunza
    - wakati wa ziara hizi
    - Ziandaliwe semina juu ya hifadhi ya ardhi na kilimo mseto.

Wakulima pia walitoa mapungufu waliyoyaona nayo ni:

- Muda wa ziara ulikuwa mfupi mno na ratiba kutokufuatwa.

### 2.1.6 Mapendekezo ya wawezeshaji

Kutokana na mapendekezo na hoja zilizotolewa na wakulima, wawezeshaji wa ziara hii ya mafunzo, wameshauri kuwa ziara zijazo ziwe na ratiba ambayo haitajumuisha mambo mengi na itoe nafasi ya kutosha kwa wakulima kujifunza zaidi. Aidha wameshauri kamati ya ufuatiliaji na uhakiki wa mradi kushiriki pamoja na kamati ya utekelezaji ya

mradi katika kufuatilia wakulima ambao walishiriki katika ziara za mafunzo na kuona kama wametekeleza waliyoahidi au kujaribu kutumia teknolojia walizojifunza katika ziara.



*Picha hii inamwonyesha Mkulima wa Lushoto akitoa maelezo juu ya kutengeneza matuta ngazi na umuhimu wake katika kuhifadhi ardhi. Mkulima huyu alichaguliwa kuwa mkulima bora wa Mkoa wa Tanga wakati wa Maonyesho ya Nane nane ya mwaka 2001.*



## 2.2. Nyanda za Juu Kusini: Uzoefu kutoka Wilaya za Njombe na Mbarali

Wakulima kutoka wilaya za Morogoro Vijijini, Kilosa na Bagamoyo walitembelea vijiji vilivyoko wilaya ya Njombe na Mbarali kuanzia tarehe 10 mpaka 12 Septemba, 2001. Dhumuni kubwa lilikuwa kubadilishana uzoefu juu ya utunzaji bora wa mifugo na samadi.

### 2.2.1 Vigezo vya kuchagua maeneo na wakulima

*Uchaguzi wa eneo*

Eneo lilichaguliwa kutokana na umuhimu wake na mada iliyopendekezwa wakati wa warsha ya pili ya wakulima wa Kanda ya Mashariki iliyofanyika Mikumi, Juni 2001, yaani matatizo yanayowakabili wakulima wa maeneo ya ukame kiasi kuhusu rutuba ya ardhi, matumizi ya mbolea ya samadi na wanyama kazi.

*Uchaguzi wa wakulima*

Wakulima 12 walichaguliwa kwa kutumia vigezo vifuatavyo: ubunifu; uhusiano na vikundi au vyama vya wakulima; uwezo wa kushirikiana na wengine na jinsia. Msafara huo ulijumuisha pia; washauri wa ugani watatu kutoka wilaya za Morogoro Vijijini, Bagamoyo na Kilosa; watafiti watatu kutoka

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo; mtafiti mmoja kutoka SECAP Lushoto na mmoja kutoka ARI Ilonga.

### 2.2.2 Matokeo

Wakulima wageni walipata nafasi ya kushiriki kwa vitendo kwenye shughuli za kilimo endelevu, utunzaji wa mifugo, hifadhi ya maliasili na maisha ya kisasa na asilia ya watu wa wilaya za Njombe na Mbarali. Waliweza kuona mbinu na njia mbali mbali za kilimo na ufugaji bora, kati ya mambo muhimu waliyoona ni kama yafuatayo:

- Zana mbali mbali za wanyama kazi kama vile jembe la kulimia, jembe la palizi na jembe la kufukua mistari na kutengeneza matuta
- Utunzaji bora wa mifugo bandani na wa uchungaji holela
- Makazi ya wachungaji (Wamasai, Wabarbaig, Wasangu na Wasukuma)
- Ulimaji wa kilimo kisichotifua ardhi, pamoja na matandazo hai kwa kutumia mimea jamii ya mikunde kama mazao ya kuhifadhi ardhi.
- Utumiaji na utunzaji samadi
- Ghala za kuhifadhia nafaka (Vihenge)
- Mabanda ya mifugo
- Utumiaji wa mimea asili yenye manufaa kwa kilimo na mifugo
- Utunzaji wa vitalu vya miche ya miti
- Mifereji ya asili ya umwagiliaji



- Teknolojia mbali mbali za kuhifadhi ardhi kama vile makinga maji na kilimo mseto.

### 2.2.3 Mafunzo

Kutokana na mambo mengi wakulima waliyoyaona, wamejifunza yafuatayo:

- Njia bora za kutumia na kutunza samadi
- Umuhimu wa kutumia wanyama kazi kwa kulima, kupalilia na kutengeneza matuta
- Umuhimu wa kutumia madawa yatokanayo na mimea ya asili kwa shughuli za kilimo na mifugo kama vile, kudhibiti magugu, magonjwa na wadudu
- Umuhimu wa vikundi vya wakulima ili kuwawezesha kupata na kumiliki teknolojia na soko la maziwa
- Umuhimu wa kufugia bandani
- Utunzaji bora wa mifugo
- Umuhimu wa kuvuna maji kwa ajili ya umwagiliaji
- Kilimo bora cha mpunga
- Ushirikiano imara kati ya wakulima, watafiti na washauri wa ugani katika kusambaza teknolojia

Wakulima wenyeji kwa upande wao walishauriwa na wakulima wenzao kuhusu dhana muhimu za kilimo na ufugaji bora. Jumuia za wafugaji wa Mbarali walipewa changamoto na wafugaji wenzao kutoka Bagamoyo, kuwa wapunguze idadi ya mifugo, wapeleke watoto wao shuleni na wawe na makazi ya

kudumu kuliko kuhamahama na mifugo yao na pia wajenge nyumba bora.

### 2.2.4 Mipango ya utekelezaji ya wakulima

Wakulima wageni walionyesha utashi na ari kubwa ya kujifunza muda wote wa ziara ya mafunzo. Kwa nyakati mbali mbali, walionekana kuuliza maswali au kushiriki kikamilifu katika majadiliano, vyote vikiwa katika kupata maelezo na ujuzi zaidi wa teknolojia zinazotumiwa na wenyeji wao. Wakulima hao, wageni waliazimia na kuahidi kutumia ujuzi walioupata ili kuboresha maisha yao. Hivyo watakaporudi makwao wameahidi kufanya yafuatayo:

- Kutunza na kutumia samadi
- Kujenga mabanda bora ya mifugo na sehemu za kutunzia mbolea
- Kununua na kutumia zana zinazokokotwa na wanyama kazi
- Kuwafundisha maksai jinsi ya kukokota zana zinazokokotwa na wanyama kazi
- Kupanda na kutumia mimea asili ya manufaa kwa kilimo na mifugo
- Kujenga nyumba bora za kuishi
- Kuvuna maji kwa ajili ya umwagiliaji na mifugo
- Kujenga ghala za kuhifadhia nafaka
- Kutengeneza makinga maji na kupanda malisho





*Picha hii ni mfano wa nyumba bora za mifugo zenye gharama nafuu. Picha ilichukuliwa huko Itulike, Njombe.*

### 2.2.5 Hoja zilizojitokeza/zilizotolewa

Wakulima wageni walitoa hoja mbali mbali zenye lengo la kuboresha ziara za mafunzo na pia kuwezesha wakulima kujifunza zaidi kutokana na ziara hizo. Kwa ujumla, ziara ilikuwa ya mafanikio makubwa kwa wote wageni na wenyeji wao. Hata hivyo, wageni walitoa mapendekezo yafuatayo:


- Kuwe na ziara zaidi za mafunzo

- Uwezekano wa kupatiwa mtaji na mikopo ya ng'ombe wa maziwa kutoka mradi wa kimataifa wa mitamba (HPI) uangaliwe
- Ratiba ya ziara ipangwe kiasi kwamba wakulima wachache wenye teknolojia zinazofanana watembelewe ili kuokoa muda
- Muda uliopangwa haukutosha kuona mambo yote pamoja na majumuisho
- Watafiti na washauri wa ugani wawatembelee wakulima wa kanda ya mashariki kutathmini utekelezaji wa mambo waliyojifunza.

### 2.2.6 Mapendekezo yaliyotolewa na wawezeshaji wa ziara

Ili kuweza kufuatilia mafanikio waliyoyapata wakulima baada ya ziara au kutathmini matokeo ya ziara, wawezeshaji wameshauri kuwa M&E na ziara za mafunzo zitumike kutathmini kiwango cha utekelezaji. Walishauri zaidi kuwa IAT ishirikishwe katika zoezi la ufuatiliaji.





*Mkulima wa Ibumila, Njombe akionyesha namna ya kuchota maji kwa ajili ya umwagiliaji toka kwenye kisima nyumbani kwake.*

## 3.0 Hitimisho

Kwa ujumla ziara hizi za mafunzo kati ya kanda na kanda zimekuwa za mafanikio kwa wahusika wote, yaani wakulima wageni na wenyeji katika maeneo yao. Imedhihirika kuwa wakulima hujifunza zaidi kwa kuona na kushirikiana kimawazo na kimatendo na wakulima wenzao wenye malengo yanayofanana na tamaduni sawia.

Kwa upande wa Kanda ya Mashariki wakulima wageni na wenyeji walifaidika kwa pamoja kutokana na ziara hiyo. Kwa wale wa Nyanda za Juu Kusini ilitokea kuwa wageni ndio walifaidika zaidi kuliko wenyeji. Huenda hii ilitokana na kuwa wakulima wa vijiji vya wilaya ya Njombe wamekuwa na teknolojia ambazo ni ngeni sana kwa wakulima wageni na hivi kutokuwa na kubadilishana uzoefu ipasavyo.

Tukichukulia kuwa hii ni mara ya kwanza kwa ziara za mafunzo za wakulima kufanyika kati ya kanda na kanda, uchaguzi wa mada ndio msingi wa mafanikio. Kwa bahati nzuri uchaguzi wa mada katika sehemu zote mbili ulikuwa sahihi na hivyo kufanikisha.

Ni matarajio ya wawezeshaji wa ziara kuwa watekelezaji wote wa mradi na washika dau wengine watatilia mkazo umuhimu wa kuwashirikisha wakulima wenye tamaduni na malengo sawia katika upokeaji wa teknolojia. Kwa mfano, katika ziara hizi, wachungaji kutoka Kanda ya Mashariki



walishirikiana na wenzao wa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini.



*Picha hii inaonyesha kihenge cha kuhifadhia mazao, kama njia mojawapo ya kuboresha uhakika wa chakula. Picha ilichukuliwa kwa mkulima wa Mbarali.*